

Mawasiliano kwa Kiswahili

Maswali Yanayoulizwa Mara kwa mara

Kujifunza Nyumbani – Wanafunzi Wapya

1. Je, mwanangu atahitajika kurudia mwaka wa shule au kozi yoyote?

Janga hili halipaswi kuathiri elimu ya mtoto wako. Wanafunzi wote waliokuwa wakifaulu kabla ya shule kufungwa wanapaswa kuingia gredi inayofuata au kupewa alama zao. Ikiwa sivyo, mfanyakazi wa shule atawasiliana nawe ili kujadili hali ya mtoto wako.

2. Je, kuna mpango wa ujifunzaji unaoandaliwa kwa ajili ya wanafunzi?

Ndio, walimu watawasiliana na kila mwanafunzi wao ili kutekeleza mpango kwa ajili ya kuhakikisha kwamba ujifunzaji wao unaendelea. Mipango itazingatia uwezo na mahitaji maalum ya kila mwanafunzi.

Aida, tovuti hii jemeduque.ca inapendekeza baadhi ya shughuli za kielimu kwa ajili ya wazazi na wanafunzi.

Maelezo mafupi ya matarajio

Gredi	Shabaha ya muda	Masomo makuu yaliyoathiriwa
K - 2	Saa 1 + dakika 30 za kusoma + dakika 30 za shughuli nyingine ya kimwili	Kusoma Hesabati
3 - 5	Saa 1 + dakika 30 za kusoma + dakika 30 za shughuli nyingine ya kimwili	Kusoma Hesabati Sayansi
6 - 8	Masaa 2 + dakika 30 za kusoma + dakika 30 za shughuli nyingine ya kimwili	Kusoma Hesabati Sayansi Sayansi ya Jamii
9 - 10	Masaa 2.5 + dakika 30 za kusoma + dakika 30 za shughuli nyingine ya kimwili	Kusoma, kuandika, Kifaransa Hesabati Kozi nyingine kwenye muhula Mwendelezo wa kozi za mtandaoni kama amejiunga
11 – 12	Masaa 2.5 + dakika 30 za kusoma + dakika 30 za shughuli nyingine ya kimwili	Kusoma, kuandika, Kifaransa Hesabati Kozi nyingine kwenye muhula Mwendelezo wa kozi za mtandaoni kama amejiunga

3. Je, mtoto wangu wa chekechea atapewa ripoti nyingine kwa mwaka wa shule 2019-2020?

Hapana, kwa sababu zifuatazo, hakuna ripoti zitakazotolewa tena katika ngazi ya chekechea kwa mwaka wa shule 2019-2020.

- Walimu wengi hawakupata nafasi ya kupima maendeleo ya wanafunzi wao wote au kuingiza chunguzi hizi kwenye mfumo wa usimamizi wa matokeo kabla ya shule kufungwa.
- Kwa sababu wanafunzi wengi hawawezi kufanya kazi zao za shule wakiwa nyumbani tangu katikati ya mwezi Machi mpaka mwishoni mwa mwaka wa shule kwa sababu kadhaa (zinazohusiana na familia, muunganisho wa Intaneti, nk.), walimu hawatafanya upimaji wowote ulio rasmi wa maendeleo na utendaji wa wanafunzi.

Maelezo yatawekwa chini kwenye ripoti ya mwisho ya maendeleo (R1 – Desemba 2019) ndani ya faili la mwanafunzi, yakiashiria kwamba mwaka wa shule ulikalizwa, na hakuna ripoti nyingine itakayotolewa kwa mwaka wa shule 2019-2020.

Tafadhali muulize mwalimu wa mtoto wako maswali na wasiwasi mwingine wowote kuhusu maendeleo na utendaji wa mtoto wako.

4. Kwa kuwa shule zimefungwa, mtoto wangu atawezaje kufikia matarajio katika mwaka ujao wa shule?

Ni muhimu kushirikiana na mwalimu kadri iwezekanavyo ili kuhakikisha kwamba ujifunzaji unaendelea nyumbani ilhali shule zikiwa zimefungwa.

Mwanzoni mwa mwaka ujao wa shule, walimu wataandaa wasifu wa darasa lao na kurekebisha uwekaji wao mipango ili uakisi mahali walipofikia wanafunzi katika ujifunzaji wao.

5. Je, mtoto wangu wa Gredi 12 atahitimu?

Wanafunzi wote waliokuwa njiani kuhitimu watapokea vyeti vyao. Ikiwa sivyo, mfanyakazi wa shule atawasiliana nawe ili kujadili hali ya mtoto wako.

6. Je, mtoto wangu wa sekondari ngazi ya juu atapewa ripoti nyingine kwa mwaka wa shule 2019-2020?

Ndio, mwishoni mwa mwaka wa shule, mtoto wako atapewa ripoti ya mwisho. Haya ndiyo yanatayokuwa kwenye ripoti hiyo:

- Matokeo ya kila kozi ambayo mtoto wako ameikamilisha katika mwezi Januari (kozi ya muhula wa kwanza).

- Isipokuwa katika hali zisizo za kawaida, alama hii CIC (alama ya kozi isiyokamilika) itaonekana kwenye kila kozi iliyoanza mwezi Septemba au mwishoni mwa mwezi Januari lakini haikukamilishwa kwa sababu shule zilifungwa (kozi za muhula wa pili na kozi za mwaka mzima).
- Maelezo ya chini yanayosema, *“Kwa sababu ya kufungwa kwa shule kulikosababishwa na COVID-19, mwanafunzi huyu alipewa alama ya CIC (alama ya kozi isiyokamilika) ili kuashiria kwamba mwanafunzi huyu alipewa alama ya kozi ingawa si matakwa yote ya kozi yalifikiwa.”*
- Wastani wa jumla kwa mwaka unaoendelea ambao unaakisi tu matokeo yaliyofikiwa mpaka kufikia mwishoni mwa mwezi Januari 2020 (kozi ya muhula wa kwanza na nusu ya kwanza ya kozi za mwaka mzima).

Ripoti ya mwisho ya mtoto wako itapatikana kwenye tovuti ya [Wazazi/wanafunzi](#).

7. Je, taasisi za elimu ya juu ambazo mtoto wangu wa Gredi 12 ametuma maombi zitapokea nakala ya cheti cha mtoto wangu?

Ndio, nakala za vyeti zitatumwa kwa taasisi za elimu ya juu kama kawaida.

8. Je, kutakuwa na sherehe na shughuli za mahafali?

Kadri itakavyowezekana, baadhi ya matukio yatafanyika. Hata hivyo, yumkini haitawezekana kufanya sherehe kama zile ambazo zimefanywa katika miaka iliyopita. Utapewa taarifa zaidi kuhusu matukio yanayoweza kufanywa na tarehe, pamoja na maelezo kuhusu namna matukio haya yatakavyofanyika.

9. Mtoto wangu yupo Gredi 12. Je, mtoto wangu ataweza kujifunza masomo ya elimu ya juu mwaka ujao?

Taasisi zote za elimu ya juu nazo pia zimeathiriwa na COVID-19 na zitahitajika kuandaa mpango wa mpito ili ziweze kukabiliana na uhalisia huu. Taasisi za elimu ya juu za New Brunswick zimesema kwamba kufungwa kwa shule hakutaathiri uandikishaji wa wanafunzi.

Maelezo zaidi kuhusu mipango ya mpito yatatolewa wiki chache zijazo.

10. Je, inawezekana kufika shuleni ili kuchukua vitu binafsi vya mtoto wangu?

Katika wiki chache zilizopita, wanafunzi na wazazi wao wamepata fursa ya kuja kuchukua vitu binafsi na zana za kiteknolojia zilizoachwa shuleni. Kama bado hujaweza kufanya hivi, tafadhali tuma barua pepe kwenda shule ya mtoto wako au acha ujumbe wa simu ili uweze kupata taarifa na maelekezo zaidi.

11. Ipi ni miongozo ya kufuata wakati wa kutumia zana za kiteknolojia za Idara husika?

Wanafunzi wanaoazima zana ya kiteknolojia kutoka Idara husika au shuleni wanapaswa kufuata miongozo hii:

- Tumia zana ya kiteknolojia kwa madhumuni ya kielimu tu.
- Tunza kifaa hicho cha kiteknolojia na waya wake wa umeme.
- Usipakue progamu au michezo kwenye kifaa husika.
- Rudisha kifaa hicho cha kiteknolojia mara shule zikifunguliwa.
- Tii Sera katika 311 – [Matumizi ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano](https://www2.gnb.ca/content/gnb/biling/eecd-edpe.html) ya Idara ya Elimu (<https://www2.gnb.ca/content/gnb/biling/eecd-edpe.html>).

12. Nifanye nini ili kumsadia mtoto wangu aendelee kujifunza kama hatuna huduma ya Intaneti nyumbani?

Ili kuzisaidia familia kuendeleza ujifunzaji wa watoto wao, Serikali ya New Brunswick imechukua uamuzi wa kutoa huduma ya Intaneti kwa nyumba ambazo hazijaunganishwa. Hatua zinaendelea kuchukuliwa ili kuziunganisha nyumba hizi na mtandao wa intaneti.

13. Napaswa kwenda wapi kwa taarifa zaidi kuhusu kufungwa kwa shule?

Unaweza kupiga namba ya bure ya Idara ya Elimu na Makuzi ya Awali ya Watoto kupitia 1-844-288-3888 (7 a.m. mpaka 9 p.m., Jumatatu mpaka Alhamisi; 7 a.m. mpaka 5 p.m., Ijumaa, na 8 a.m. mpaka 4 p.m., Jumamosi na Jumapili). Unaweza pia kutembelea tovuti ya wilaya kwa habari zote mpya.